

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MAGOLE  
S.L.P 1191  
MOROGORO  
0714201958/076496555**

KUMB NA:MGSS/ED/ JOIN/2021

Ndg.....  
SLP .....

**YAH: MAAGIZO YA MWANAFUNZI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAGOLE  
MWAKA WA MASOMO 2021.**

1.0.Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kijiungu kidato cha kwanza (I) katika shule hii mwaka wa masomo 2021. Shule ya sekondari MAGOLE lipo kijiji cha Magole A, 4km kutoka barabara kuu ya Dodoma –Morogoro,upande wa kushoto kwenye barabara iendayo Turiani.(kibao cha kuitambulisha shule kipo jirani na mahakama ya Mwanzo Magole). .Muhula wa kwanza wa mwaka wa masomo utaanza tarehe 04/January/2021,Unatakiwa kuripoti shulenii tarehe 04/January/2021 siku ya Jumatatu. HONGERA SANA KWA KUCHAGULIWA.

**2.0.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KABLA YA KUFIKA SHULENI.**

Soma maelekezo yaliyoko kwenye barua hii kikamilifu na uyazingatie na kuyatekeleza kabla ya kufika shulenii.

**2.1.SARE YA SHULE**

**WAVULANA:**

- (a) Suruali 2 rangi kijani yamgomba/blue nyeusi mzunguko wa chini **uwe cm 16 au zaidi,modal haziruhuswi.**
- (b) Shati 2 rangi nyeupe mikono mifupi yawe ya kuchomekea.
- (c) Soksi nyeusi jozi 2 au zaidi
- (d) Viatu vyeusi jozi mbili au zaidi viwe vya kufunga na kamba.
- (e) Bukta 2 za michezo ragi blue
- (f) T-shirt 2 za rangi ya DARK BLUE t-shirt kwa shughuli za kimasomo

**WASICHANA:**

- (a) Sketi 2 rangi ya kijani ya mgomba/dark blue sketi zishonwe za **kuvuka magoti.**
- (b) Shati 2 rangi nyeupe mikono mifupi ziwe za kuchomekea.
- (c) Soksi (Stocks) nyeupe jozi mbili au zaidi
- (d) Viatu vyeusi jozi mbili au zaidi viwe vya kufunga na kamba
- (e) Nguo za michezo track suit nyeusi jozi mbili
- (f) T-shirt 2 za rangi ya dark blue kwa shughuli za darasani

### **ADA NA MICHANGO YA SHULE.**

- (a) Ada yote itagharimiwa na Serikali.
- (b) Mahitaji binafsi ya mwanafunzi kama Daftari, begi la kubebea vifaa vyake,kalamu, chakula cha mchana,mathematical set na usafiri wa kwenda na kurudi shuleni ni jukumu la mzazi/mlezi mwenyewe.

### **SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE YA SEKONDARI MAGOLE.**

3.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule.
- (c) Kujisomea muda wote ukiwa shuleni na nyumbani.
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuwepo ndani ya eneo la shule wakati wa saa za masomo.
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya Shule hairuhusiwi kuwa na nywele ndefu,kufuga kucha,kupaka hina au cream kwenye ngozi ya mwili wakati wote wa uanafunzi wako.
- (g) Kuvaas sare ya shule wakati wote unapotakiwa na kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3.2 Ukipika shuleni utasomewa sheria,kanuni na taratibu za shule, na utajaza fomu maalumu na mkataba wa kutokiuka sheria hizo.

#### **4.0 Mambo mengine muhimu.**

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule/MSAJILI WA WANAFUNZI mara utakaporipoti shule.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo fujo na makosa ya jinai, ikabidhi kwa mkuu wa shule/MSAJIRI WA WANAFUNZI


(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na taratibu za shule, form hii nayo utaikabidhi .Mawasiliano na mzazi yafanyike kupitia walimu walezi na ni kinyume cha taratibu kuwasiliana na mzazi ukiwa eneo la shule bila taarifa kwa mwalimu mlezi

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAGOLE**

.....  
**FINYILISE S.ELIAS  
MKUU WA SHULE**

**KIAMBATANISHO A: FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI**

OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA NA  
**SHULE YA SEKONDARI MAGOLE.**  
(Jaza fomu hii kwa uangalifu)



1. Jina kamili la mwanafunzi .....
2. Tarehe ya kuzaliwa..... wilaya.....
3. Kabilia..... uraia .....
4. Jina la mzazi.....  
Anwani ya mzazi.....  
Kazi ya mzazi..... Simu na .....

**(sehemu hii ijazwe na wanafunzi ambao hawakai na wazazi wao)**

5. (a) Jina la mlezi .....
- (b) Uhusiano kati ya mlezi na mwanafunzi.....
- (c) Kazi ya mlezi.....simu na .....
- (d) Anwani ya mlezi.....
6. Shule ya msingi atokayo mwanafunzi.....
7. Wakati wa likizo mwanafunzi atakwenda wapi?.....
8. Maelezo ya mwanafunzi .....
9. Ujuzi (stadi) mwingine .....
10. Saini ya mwanafunzi.....  
Tarehe .....

## **KIAMBATANISHO B: FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA KUJIUNGA SHULENI**

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
SHULE YA SEKONDARI MAGOLE**

Mimi.....Msichana/mvulana  
Ninakubali kuingia kidato cha ..... katika shule ya sekondari MAGOLE  
Kama mwanafunzi wa kutwa tarehe..... Nitafika shuleni bila kuchelewa.

Nitatii sheria za shule na nitaishi maisha mazuri. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea,nitalazimika kulipa uharibifu wowote uwe ni majengo,vitabu na vitu vyote nitakavyoaharibu nikiwa shuleni.

Sahihi ya mwanafunzi..... tarehe.....

**SEHEMU YA MZAZI MLEZI:** Mimi .....ninakubali mtoto wangu  
..... Asome katika shule ya sekondari MAGOLE kuanzia tarehe.....

Nina ahidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama llivyotajwa katika barua.

Ninakuhakikisha kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule Na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za Kujitegemea.

Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubaliwa kuingia katika shule ya Sekondari MAGOLE kama mwanafunzi wa kutwa.hivyo muda wa mwanafunzi kuwa shuleni ni saa 1 asubuhi hadi saa 10 Jion, na nitawajibika kwa malezi ya ziada kwa muda ambao si wa masomo na siku za mapumziko.

Anwani yangu ya kudumu ni :-

.....  
simu .....

Sahihi..... tarehe.....

**KIAMBATANISHO C: UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA AU CHETI CHA  
KUZALIWA.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MKUU WA (W)  
WILAYA YA KILOSA  
S.L.P 8  
KILOSA

..../JANUARY/2021

MKUU WA SHULE,  
SHULE YA SEKONDARI MAGOLE  
S.L.P 1191  
MOROGORO

**UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA**

Nathibitisha kuwa.....  
(Jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/ kwa  
kuandikishwa).

Baba yake (Jina kamili)..... wilaya ya .....,  
Amezaliwa katika mkoa wa ..... Kata ya .....

Mama yake (Jina kamili)..... wilaya ya .....,  
Amezaliwa katika mkoa wa ..... kata ya .....

**MKUU WA WILAYA**

**NB:**

*Kama mwanafunzi ana cheti cha kuzaliwa taarifa za form hii isijazwe alete kopi ya cheti cha  
kuzaliwa.*

## **APPENDIX D: MEDICAL EXAMINATION FORM**

### **PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

MAGOLE SECONDARY SCHOOL.

P.O. BOX 1191  
MOROGORO.

...../JANUARY/2021

#### **PART A**

Mr. /Miss .....

Please examine the above named student as to his/her physical and mental Fitness for full time student in this school. The examination should include the following categories:-

01. Hemoglobin .....
02. P.V. bleeding .....
03. Sight.....
04. Blood pressure .....
05. Urine for sugar .....
06. Stool for routine examination.....
07. Pregnancy test .....
08. Skin diseases.....
09. Leprosy .....
10. Any deformity.....
11. Epilepsy.....
12. Pulmonary tuberculosis.....
13. Neurosis .....
14. Venereal diseases.....
15. Other serious diseases.....

#### **PART B.**

(To be completed by a Government Medical Officer )

1. I have examined the above named student and consider that he/she is Physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time schooling.
  2. Other Comments .....
  3. Date.....JANUARY/2021      Signature .....
- Station..... Designation.....

Official stamp.....

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI  
SHULE YA SEKONDARI MAGOLE**

**SHERIA ZA SHULE YA SEKONDARI MAGOLE (BY LAWS).**

1. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria siku zote za masomo yaani wiki 20 kwa mhula au wiki 40 kwa mwaka mzima bila kukosa.Ruhusa za simu haziruhusiwi.
2. Mwanafunzi hapaswi kuharibu mali ya umma na kama ikibainika ameharibu mali ya umma kwa makusudi atawajibika kuilipia mara mbili ya uharibifu huo pamoja na hatua nyingine za kisheria.
3. Mwanafunzi anapaswa kuwahi asubuhi saa 1 kamili alfajiri na kuondoka shuleni saa 10 jioni.
4. Baada ya miaka minne wazazi wana hiyari ya kuwafanyia mahafali vijana wao,gharama za mahafali ni za wazazi mahafali siyo lazima, ingawaje ni tukio la shule,na mavazi rasmi ya siku ya mahafali ni uniform ya shule.
5. Uniform ni vazi la shule isivaliwe nje ya shughuli za shule. Mwanafunzi akiwa nyumbani asivae uniform za shule Sare za shule zibaki kwa matumizi ya shule tu.
6. Siasa za vyama haziruhusiwi shuleni, ukibainika utachukuliwa hatua kali za kisheria ila mwanafunzi unaruhusiwa kuijunga na scout.
7. Utoro wa mara kwa mara ni mwiko ,mwanafunzi akifikisha siku tisini za utoro atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.
8. Wanafunzi wanaopanga mitaani watakaguliwa na matroni/patroni kuangalia mwenendo wa nidhamu zao,aidha mzazi unashauriwa kumtembelea mara kwa mwanafunzi aliyepanga chumba.
9. Kutakuwa na shughuli za uzalishaji mali na elimu ya kujitegemea hapa shuleni, kila mwanafunzi anapaswa kushiriki kikamilifu shughuli hizi.

10. Ni muhimu Wazazi kufika mara kwa mara shulen ikuangalia tabia na mwenendo wa wanafunzi wao.
11. Maamuzi ya vikao vya wazazi yapoafikiwa kwenye mukutano halali wa wazazi shulen, itakuwa ni sheria kwa wanafunzi wote, hivyo wazazi mnashauriwa kuhudhuria vikao vya wazazi kwa ajili ya maamuzi, usipofika siku ya kikao cha wazazi utalazimika kufuata kilichokubaliwa na wazazi wote.
12. Ni marufuku kukatiza njia zisizo rasmi(tress pass) katika eneo la shule, hatua za kinidhamu zitachukuliwa.
13. Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana kwenye mabanda ya video na kwenye vigodoro bila idhini ya shule kama nyumbani kwao kuna shughuli hiyo taarifa itolewe shulen i.
14. Mwanafunzi awapo shulen i haruhusiwi kumiliki simu ya aina ye yote, redio na kifaa chochote kinachotumia umeme akionekana navyo atanyang'anya na hatarudishiwa na hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.
15. Kandambili au viatu vya wazi haviruhusiwi shulen i, kama kuna ulazima mwalimu mwandamizi malezi na utamaduni atatoa kibali cha muda.
16. Muda wa masomo mwanafunzi hataruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule na akibainika ataadhibiwa.
17. Mzazi aliyeandikishwa jina shulen i ndiye mzazi anayeruhusiwa kuja shulen i kwa shughuli za malezi au wito shulen i.
18. Mzazi ukifika eneo la shule si ruhusa kuingia madarasani au kuongea na mwanao bila idhini ya shule kufanya hivyo ni kukiuka sheria na mwanao atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.
19. Ni mwiko kwa mtu asiyehusika kufika eneo la shule bila sababu za msingi, eneo la shule ni eneo la kitaaluma, mambo mengine wasiliana na mwanao ukiwa nyumbani.

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI  
SHULE YA SEKONDARI MAGOLE**

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE  
SHULE. (LAWS)**

- 1) Wizi wa aina yeote ile
- 2) Uasherati, ubakaji na ushoga
- 3) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- 4) Uvutaji sigara na bangi
- 5) Makosa ya jinai
- 6) Kupigana au kupiga
- 7) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- 8) Kudharau Bendera ya Taifa
- 9) Kuoa au kuolewa
- 10) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- 11) Kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba
- 12) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu na Kukataa adhabu kwa makusudi.

**MAENEKO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUYATEMBELEA  
BILA KIBALI MAALUMU(LAWS)**

1. Chumba cha walimu (staff room)
2. Ofisi za shule
3. Maabara
4. Jikoni
5. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
6. Vilabu vya pombe
7. Majumba ya starehe
8. Majumba ya kufikia wageni.

ASANTE

.....  
**FINYILISE S.ELIAS  
MKUU WA SHULE.**